# Uelewa na ushiriki wa wazalishaji wadogo katika mchakato wa utwaaji wa ardhi kwa ajili ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki: Uchunguzi kifani wa Wilaya ya Kilindi, mkoa waTanga, Tanzania.

HakiArdhi

Juni 2024

## Muhtasari

Ardhi na rasilimali zilizopo katika ardhi ni muhimu sana kwa wazalishaji wadogo nchini Tanzania ambao ni wakulima na wafugaji hususan wanawake kwa sababu ndipo wanapopata mahitaji ya kila siku ya kijamii na kiuchumi kama vile makazi, chakula, malisho na kuongeza kipato. Kwa mujibu wa Sheria za Ardhi, ardhi yote nchini mali ya umma, na Rais ndiye mdhamini kwa niaba ya wananchi wote. Mfumo wa Sheria za Ardhi unampa Rais mamlaka ya kutwaa ardhi kutoka katika kundi lolote la ardhi, iwe ya jumla, kijiji, au hifadhi, kwa maslahi yoyote ya umma kupitia Utwaaji Ardhi wa Lazima. Serikali inachukulia utwaaji wa ardhi wa lazima katika kufanikisha maslahi ya umma ambayo ni pamoja na uwekezaji. Hata hivyo, utwaaji wa lazima wa ardhi ni muhimu usimamiwe ipasavyo kwasababu husababisha ukiukwaji wa haki ya matumizi na umiliki wa ardhi miongoni mwa wazalishaji wadogo na kusababisha umaskini miongoni mwao.

Matokeo ya utafiti yanayowasilishwa katika ripoti hii yanatokana na tathmini ya uelewa na ushiriki wa wazalishaji wadogo katika mchakato wa utwaaji wa ardhi kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki. Mradi huu unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litakalofukiwa na kuvuka mpaka ili kusafirisha mafuta ghafi kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda hadi Chongoleani mkoa wa Tanga, nchini Tanzania katika mwambao wa mashariki mwa Tanzania, ambako yatasafirishwa kwenda kwenye masoko ya kimataifa. Urefu wa bomba hilo ni kilomita 1,450, kati ya hizo takriban kilomita 1,147 (80%) zitakuwa nchini Tanzania na litapita katika mikoa 8 na wilaya 25.

Utafiti huu ulifanyika katika vijiji viwili vya Lekitinge na Mkindi katika wilaya ya Kilindi mkoani Tanga; ambapo jumla ya ekari 318.98 za ardhi zimetwaliwa ili kuruhusu shughuli za ujenzi wa bomba la mafuta na kambi zitakazotumika wakati wa ujenzi wa bomba hilo. Mchakato wa utwaaji ardhi ulifuata mfumo wa kisheria wa nchini Tanzania hususan Sheria za Ardhi namba 4 na 5 za mwaka 1999 na Sheria ya Utwaaji Ardhi namba 47 ya mwaka 1967 ambayo inampa Rais mamlaka ya kutwaa ardhi kutoka katika kundi lolote, ambapo katika mradi huu ardhi kubwa iliyotwaliwa inatoka katika kundi la ardhi ya kijiji. Vile vile, kulikuwa na matumizi ya Viwango vya Kimataifa vya Ufadhili vilivyotumika katika kugharamia faida nyinginezo katika fidia kama vile kuhuisha kipato na usambazaji wa chakula kwa familia zilizoathiriwa na mradi.

Pia ilibainika kuwa kulikuwa na ushiriki mdogo wa taasisi katika ngazi ya Serikali za Mitaa zilizopewa mamlaka ya kusimamia ardhi ya kijiji kama vile Idara ya Ardhi ya Halmashauri ya Wilaya, halmashauri ya kijiji na mkutano mkuu wa kijiji ingawa nyaraka rasmi za mradi wa bomba la mafuta zinaeleza kuwa mchakato wa utwaaji ardhi ni shirikishi ingawa kiuhalisia kwa kiasi kikubwa utaratibu wa utwaaji wa ardhi ulitawaliwa na makampuni binafsi.

Vile vile, hapakuwa na mafunzo ya kujenga uelewa juu ya masuala ya sheria za ardhi na haki za ardhi kwa waathirika wa mradi, wanavijiji wasio waathirika na viongozi wa vijiji kabla au wakati wa mchakato wa utwaaji wa ardhi. Kilichobainika ni kuwa timu ya utekelezaji wa utwaaji wa ardhi ilikuwa ikitoa ufafanuzi wa ukokotoaji wa mahesabu ya fidia na malipo kwa waathirika wa mradi pekee. Wanavijiji ambao mashamba yao yasingeathiriwa na mradi hawakualikwa kwenye mijadala hii kwa kupuuza ukweli kwamba ardhi katika ardhi ya kijiji inatumika na kumilikiwa kijumuiya hivyo pale mwanakijiji mmoja anapoathirika maana yake jamii nzima inakuwa imeathirika.

Pamoja na mapungufu yaliyobainishwa, mpaka kufikia wakati wa utafiti huu tayari waathirika wote wa mradi walishalipwa fidia ya fedha. Stahiki ambazo bado hazikuwa zimelipwa ni pamoja na utoaji wa faida nyingine kwa mujibu wa viwango vya kimataifa kama vile ugawaji wa chakula maarufu kama kapu la chakula na ujenzi wa nyumba mbadala kwa waathirika wa mradi waliopoteza nyumba zao. Vile vile, ilibainika kuwa waathirika wa mradi walikuwa na maswali kuhusu fomula zilizotumika katika kukokotoa kiasi cha fidia; pia waathirika wa mradi walikosoa matumizi ya kanuni ya bei ya soko katika ulipaji wa fidia ya ardhi kwasababu haitoi fidia toshelevu kwa wao kuweza kununua ardhi nyingine ili kuendeleza shughuli zao za maisha. Pia, jamii ya Wamaasai walieleza kutoridhishwa na kutokuwepo kwa fidia ya miti ya asili inayozalisha dawa za kienyeji na chakula cha binadamu na wanyama. Vile vile, walikosoa kutozingatiwa kwa ulinzi wa rasilimali nyingine za wafugaji kama vile maeneo ya malisho ya jumuiya.

Aidha, kuhusu taratibu za kukusanya na kusimamia malalamiko, waathirika wa mradi walisema kuwa walikuwa wakitumia huduma ya simu ya bure kuwasilisha malalamiko

yao kuhusu mchakato wa utwaaji wa ardhi na kuuliza maswali mengine kuhusiana na mradi wa bomba la mafuta lakini walikuwa hawapati usikilizwaji unaoridhisha na hata pale masuala yao yaliposhughulikiwa, yalishughulikiwa nje ya muda. Halikadhalika, uwasilishaji mwingine wa malalamiko ulikuwa kupitia barua pepe kama njia mbadala katika kuwasilisha madai ingawa hakuna muathirika wa mradi aliyetumia njia hii ya barua pepe kwasababu hakuna aliye na akaunti ya barua pepe.

Aidha, kuhusu uwazi na uhuru wa kujieleza ilibainika kuwa waathirika wa mradi na wanavijiji wengine hawakuruhusiwa kuhoji au kukosoa taratibu za utwaaji ardhi na walipojaribu kufanya hivyo walikumbushwa kuwa ardhi yote ni mali ya Rais, hivyo iwapo serikali inataka ardhi kwa maslahi ya umma, hakuna namna ya kupinga. Ingawa ni sahihi kwamba Rais anaweza kutwaa ardhi yoyote wakati wowote kwa mradi wowote unaoonekana kuwa muhimu kwa taifa, ni muhimu kuzingatiwa kwa taratibu za kisheria, ikiwa ni pamoja na ushirikishwaji wa waathirika wa utwaaji wa ardhi na wadau wengine; vile vile yafanyike malipo ya fidia ambayo ni kamili, ya haki na kwa wakati.

Kuhusu athari za mradi kwa jamii, ni mapema mno kutaja athari chanya za mradi wa bomba la mafuta katika vijiji vilivyofanyiwa utafiti, kwasababu kazi za ujenzi wa bomba bado hazijaanza. Aidha, bado waathirika wa mradi hawajapokea fidia nyingine walizoahidiwa ambazo zingewanufaisha, kama vile msaada wa chakula, mafunzo ya ufugaji wa kisasa, na matengenezo ya miundombinu kama barabara, vituo vya afya, vituo vya maji safi, mabwawa ya kunyweshea mifugo na majosho ya ng'ombe. Kwa upande wa athari hasi, wahojiwa wengi walihofia uhaba wa chakula na malisho kwa mifugo kwasababu miongoni mwa waathirika wa mradi kuna ambao wamepoteza ardhi yote au sehemu kubwa ya ardhi ya kilimo na ufugaji waliyotumia kwa uzalishaji wa chakula kabla ya utwaaji.

Kutokana na matokeo ya utafiti yaliyowasilishwa katika ripoti hii, yafuatayo ni baadhi ya mapendekezo ambayo yatasaidia kuhakikisha kwamba michakato ya utwaaji wa ardhi inawahusisha ipasavyo wadau wote katika hatua zote na wadau hao wanatimiza wajibu na majukumu yao. Vile vile, kuongeza uelewa wa wajumbe wa mkutano mkuu wa kijiji na halmashauri ya kijiji ili wawe na uwezo wa kushiriki katika mchakato wa utwaaji ardhi kwa maslahi yao na kijiji kwa ujumla. Mapendekezo mengine ni kufanya marekebisho ya mfumo wa kisheria kuhusu fidia ili kujumuisha vipengele zaidi ambavyo vina manufaa ya kijamii na kiuchumi kwa wazalishaji wadogo, na kuhakikisha kuna uwazi na ushirikishwaji wa taarifa kuhusu fomula zinazotumiwa kukokotoa malipo ya fidia.

HAKIARDHI

mawasiliano
info@hakiardhi.or.tz
tomitho@hakiardhi.or.tz

Chapisho hili ni sehemu ya mfululizo wa "Sauti za Watanzania" wa IPIS na toleo lake kuhusu *"Athari za mikakati ya utwaaji ardhi katika sekta ya uziduaji kaskazini mwa Tanzania"*

Ripoti kamili ya kifani hii inapatikana kwa Kiingereza kupitia: https://ipisresearch.be/home/capacity-enhancement/voices-from-the-south/voices-from-tanzania/

Belgium partner in development

Kwa msaada wa IPIS